

HABARI ZA DODOMA - (Habari leo)

# Narco yapunguza bei ya kondoo, mbuzi kuelekea Krismasi

Na Sifa Lubasi

KATIKA kuelekea Sikukuu ya Krismasi na mwaka mpya, Serikali imetangaza punguzo la asilimia 33 ya bei ya mbuzi na kondoo waliopo katika Ranchi za Taifa (NARCO) katika msimu huu wa sikukuu ili kuhamasisha wananchi kula nyama na kuongeza wigo wa soko la ndani.

Akitangaza punguzo hilo, Ofisa Masoko wa Narco, Emmanuel Mnzava alisema Serikali imeamua kutoa ofa ya Krismasi na mwaka mpya kwa wananchi wake ambapo mbuzi 3,000 na kondoo 1,000 watauzwa kwa bei ya punguzo.

Alisema bei hiyo itakuwa katika ranchi za Kongwa (Dodoma), Ruvu (Pwani), Mkata (Morogoro), West Kilimanjaro (Kilimanjaro) na Missenyi (Kagera).

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameamua kutoa 'ofa' ya Krismasi na mwaka mpya kwa wananchi wake ambapo ofa hiyo inalenga kuhamasisha ulaji wa nyama ya mbuzi na kondoo hapa nchini na kuongeza soko la bidhaa hiyo ndani ya nchi.

Aliongeza: "Awali mbuzi mmoja katika ranchi hizi alikuwa anauzwa hadi Sh 150, 000 lakini kutokana na punguzo hili sasa watauzwa kwa Sh 120,000 hadi 100,000, kwa mbuzi na kondoo ambaye akichinjwa anatoa kilo 15 hadi 20."

Ofisa masoko huyo alitaja lengo lingine la kupunguza bei ni kuhamasisha jamii ya Watanzania katika ufugaji wa kisasa na kibiashara wa mbuzi na kondoo ili kukidhi mahitaji ya soko la kigeni pamoja na machinjio na viwanda vya nyama vilivyopo na vinavyoendelea kujengwa nchini.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa ulaji wa nyama ya mbuzi na kondoo hapa nchini bado uko chini ikilinganishwa na ulaji wa nyama ya ng'ombe ambao unaongezeka kila mwaka.

Alisema mahitaji ya nyama ya mbuzi na kondoo katika soko la nje ya nchi na machinjio na viwanda vya nyama vilivyopo na vinavyoendelea kujengwa nchini yanaongezeka, hivyo kutoa fursa la soko la bidhaa hiyo kwa wafugaji.

Kwa upande wake, Mkazi wa Chamwino, Ramadhani Kiza alisema ulaji wa nyama ya mbuzi unakuwa chini kutokana na upatikanaji wake kwa kuwa ni adimu na gharama yake ni kubwa, hivyo watu wengi kushindwa kumudu.

Alisema ni vyema serikali ikaingilia kati suala hili kwa kuwahamasisha wafugaji kufuga mbuzi kisasa na kibiashara ili kufanya nyama ya mbuzi iwe inapatikana kila mahali kama ilivyo bidhaa nyingine.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa kutushushia bei ya mbuzi na kondoo lakini tunaomba ofa hii isiwe kwa muda mfupi iwe endelevu ili kila mwananchi awe na uwezo wa kununua na kufurahi na familia yake hasa kipindi hiki ambacho watu wengi wanasherehekea mwaka mpya na Krismasi," alisema.

Mfanyabiashara wa Soko la Bonanza, Maria Issa alipongeza serikali kwa kuleta punguzo la bei kwa wakati ambao unahitajika sana na watu.

Alisema sherehe za mwaka mpya na Krismasi wananchi hununua nyama ya ng'ombe na mbuzi kwa ajili ya kusherehekea na ndugu na jamaa zao.

Scanned with CamScanner

# Wakulima wakumbwa hofu mifugo kula chumvi 'feki'

Na Thobias Mwanakatwe,
NGORONGORO

ZAIDI ya wafugaji 8,000 wa kata za Ngorongoro na Nainokanoka, wamekumbwa na hofu ya ng'ombe wao kupoteza maisha baada ya kupewa chumvi iliyochanganywa na mawe na rangi inayosababisha wanapoitumia uharisha.

Chumvi hiyo ambayo imezua utata inadaiwa imesambazwa kwa wafugaji hao na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ikiwa ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mwaka 2016.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo kwa NCAA iwe inawapa wafugaji chumvi ya kulisha mifugo pamoja na maji ili wafugaji waache kupeleka mifugo yao ndani ya Bonde la Ngorongoro ambako walikuwa wakifuata chumvi ya asili na maji katika bonde hilo ambayo inasaidia sana kwa afya za mifugo.

Hata hivyo, wafugaji wamelalamika kuwa chumvi waliyopewa wiki mbili zilizopita haina viwango na imechanganywa na mawe na rangi na mifugo yao inapotumia inaharisha hali ambayo inahatarisha afya ya ng'ombe hao.

Diwani wa Kata ya Ngorongoro, Simon Saitoti, akizungumza katika mahojiano na gazeti hili alisema hali sio nzuri kwa mifugo ya wafugaji wa kata hiyo baada ya kuitumia chumvi hiyo ambayo inadaiwa kununuliwa na NCAA kutoka nchi jirani.

Saitoti alisema katika kata yake ililetwa mifuko 900 na ilikuwa imeshasambazwa kwa wafugaji zaidi ya 5000 na kubaki sita pekee kupitia kwa wenyeviti wa vijiji na baada ya ng'ombe kuanza kuitumia wakaanza kuona dalili tofauti.

Alisema baada ya kupelekewa malalamiko na wafugaji naye alitoa taarifa kwa Ofisa Mifugo na viongozi wa NCAA na kuliitishwa kikao cha wenyeviti wa vijiji vya Kayapusi, Oloilobi na Mokilale ambacho pia kilihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala.

Saitoti alisema mfuko mmoja wa chumvi hiyo wenye ujazo wa kilo 20 walipochanganya kwenye maji walibaini kuwapo kwa mchanga na rangi ambayo ilipakwa mchanga huo hali ambayo imetia shaka ya usalama wa mifugo ya wafugaji ambayo tayari imeshatumia chumvi hiyo.

Naye Kaimu Mhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Elibariki Bajuta, alipoulizwa kwa njia ya simu kuhusu suala hilo alikiri NCAA kupokea malalamiko ya wafugaji kuhusu chumvi hiyo ambayo kila mwaka imekuwa ikisambazwa na mamlaka kwa wafugaji wa kata tatu za wilaya ya Ngorongoro.

"Malalamiko tumeyasikia, ni vitu vya kawaida tu tatizo limetokea, hii chumvi inayolalamikiwa tuliisambaza mwishoni mwa mwezi uliopita (Novemba)," alisema Bajuta alipopigiwa simu.

Kwa upande wake mtaalamu wa mifugo wa NCAA, Kilasi Mollel, alipoulizwa alisema kama jambo hilo limejulikana shirika (NCAA) italifanyia kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Mangwala alisema juzi (Jumatatu) alifika eneo la tukio katika Kata ya Ngorongoro na kuzungumza na wafugaji na kutoa agizo chumvi hiyo isiendelee kutolewa kwa wafugaji tena na wale ambao wamekwishapewa wasiipe mifugo.

Mangwala alisema hatua nyingine iliyochukuliwa na serikali ni kuchukua sampuli ya mfuko mmoja wa chumvi hiyo inayodaiwa kuwa feki ili ipelekwe kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ufanyike uchunguzi wa kisayansi. Alisema majibu ya uchunguzi huo yatakapotoka wafugaji watajulisha nini cha kufanya.

Utaratibu wa kutoa chumvi bure kwa wafugaji wa kata za Ngorongoro na Nainokanoka ulianza kutekelezwa mwaka 2017 baada ya serikali kupiga marufuku wafugaji kupeleka mifugo yao 'Ngorongoro crater'.

Scanned with CamScanner



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Ally Mwinyi (aliyevaa tai) akitazama ng'ombe wa maziwa mara baada ya kuzindua kiwanda cha Maziwa cha Jeshi la Magereza (Kingolwira Milk Product Industry), kilichopo mkoani Morogoro.

Scanned with CamScanner

# DODOMA NEWS



From DAILY NEWS Reporters in Dodoma

# NARCO calls for commercial livestock keeping to meet demand

THE National Ranching Company Limited (NARCO) has underscored the need for public engagement in commercial livestock keeping of goats and sheep in the country.

Managing Director of NARCO, Prof Peter Msoffe told journalists here yesterday that they have embarked on a special campaign to mobilize the public on the need to engage in goat and sheep commercial keeping.

He said there was an increased need of goat and mutton meat in the local and international market, thus the need to prepare livestock keepers to get ready to tap the opportunities for their improved welfare.

Prof Msoffe said NARCO have been given a special offer during this festive season from December 21 to January 10, 22 at their ranches of Kongwa,Ruvu, Mkata, Kalambo, West Kilimanjaro and Misenyi to sell their livestock.

He said during the period, 3,000 goats and 1,000 sheep species of Blackhead Persian will be sold at a reduced price of 33 per cent.

The move, he said, aimed at giving a chance to the public to know the taste of the ranches' species meat and thus develop interest in livestock keeping as well as increase local consumption of the products.

"We want to widen the local market of goat and mutton meat. and in so doing increase the number of livestock keepers to meet the demand" he insisted.

Moreover, he said, the campaign, known as the Christmas and New year Offer, wants to promote the species' livestock keeping to serve the local industries as well as those being constructed.

Prof Msoffe said the country is experiencing increased consumption of beef every year compared to mutton and goat.

"Statistics are clear on the increased consumption of beef meat among the public while the numbers are small when it comes to mutton and goat, thus the need to give the community a chance to know the taste of the other products" said Prof Msoffe

He said the offer will be available in the mentioned ranches in the regions of Dodoma, Pwani, Kagera, Morogoro,Rukwa and Kilimanjaro on the basis of first come first served .

Scanned with CamScanner

With or without the ban petty traders continue to conduct their businesses under the sign board at Kimara-Mwisho in Dar es Salaam yesterday. Photo: Correspondent Miraji Msala

By Guardian Correspondent, Kongwa

# NARCO offers price reduction on sheep and goat meat during holiday

NATIONAL ranching Company (NARCO) has called on Tanzanians to adopt modern, commercial livestock keeping practices to satisfy the foreign market demand and the country meat processing factories.

It has also offered price reduction in the holidays season to mobilise the people eat goat and sheep meat and expand the domestic market.

The remarks were made here yesterday by NARCO marketing Manager, Mnzava Emmanuel on behalf of the company's managing director Prof Peter Msoffe as he was addressing reporters.

He said it was essential for Tanzanians to engage themselves in modern livestock keeping practices to satisfy the demand of local meat factories that continue to be established countrywide.

In regard to the price reduction, Mnzava said they have decided to do so to strengthen the health of Tanzanians whereby 3,000 goats and 1,000 Blackhead Persian (BHP) sheep will be sold at 33 per cent reduction in price.

He said the price reduction will involve the company's Kongwa, Ruvu, Mkata, Kalambo, West Kilimanjaro and Missenyi ranches.

"Statistics show that goat and sheep meat eating was still low compared with cow's meat which has been on increase year after year," he said.

However, he added that the demand for goat and sheep meat in the foreign market and in the local meat factories is on increase thereby providing great opportunities to livestock keepers.

The Christmas and New year offer will begin to be provided on December 21 up to January 10 next year in the named ranches," he explained.

For his part Kongwa Ranch Manager, Elisa Binamungu said they were well set to provide the services to all the people who will come up for the offer.

"In addition to this offer, every day in our ranch we slaughter cows, we have excellent meat, and we are calling for all the people to come up to purchase our products in accordance to their needs," he added.m

Scanned with CamScanner